# CHAMA KIKUU CHA USHIRIKA LINDI MWAMBAO

**NAMBA YA USAJILI AFF-LND-LND-MC-2023-24,**

S.L.P 140 LINDI

Email:lindimwambaocoopunion@yahoo.com


**19/03/2026.**

# "TANGAZO"

## ZABUNI YA UENDESHAJI WA GHALA LA KUHIFADHIA MAZAO LA CHAMA KIKUU CHA USHIRIKA LINDI MWAMBAO-LTD 2026-2027, HOTELI TATU-KILWA&ILULU MTAMA

MWENYEKITI WA BODI YA CHAMA KIKUU CHA USHIRIKA LINDI MWAMBAO- LTD ANATANGAZA NAFASI YA KAZI YA UENDESHAJI WA GHALA LA KUHIFADHIA MAZAO KWA MFUMO WA STAKABADHI GHALANI LA CHAMA KIKUU CHA USHIRIKA LINDI MWAMBAO LILILOPO KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA YA KILWA KIJIJI CHA HOTELI TATU NA GHALA LA ILULU MTAMA LILILOPO KATIKA HALMASHAURI YA MTAMA, HIVYO MAKAMPUNI AU WENYE MAJINA YA BIASHARA NA WENYE SIFA ZIFUATAZO WANAWEZA KUWASILISHA MAOMBI YA ZABUNI KATIKA OFISI YA CHAMA KIKUU CHA USHIRIKA LINDI MWAMBAO-LTD. GHALA LITATUMIKA KUTUNZA MAZAO YA UFUTA, MBAAZI NA KOROSHO NA KUENDESHA MINADA YA MAZAO YA WAKULIMA KWA MFUMO WA STAKABADHI GHALANI.

**JEDWALI NO;1**

| NA | JINA L A GHALA | MAHALI | ZABUNI NAMBA | UWEZO WA GHALA (TANI) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | LINDI MWAMBAO COOP-LTD | HOTELI- TATU | LMCU/LD/HQ/2025-2026/NC/25 | 10,000.00 |
| 2 | ILULU -MTAMA | MTAMA-DC | LMCU/LD/HQ/2025-2026/NC/25 | 5,000.00 |

**SIFA ZA WAOMBAJI.**

1. Mwombaji awasilishe barua ya maombi ya zabuni.
2. Mwombaji aambatanishe nakala ya Leseni hai ya biashara(Active business licenses)
3. Mwombaji aambatanishe nakala ya namba ya utambulisho wa mlipa kodi (TIN Number)

4. Mwombaji aambatanishe nakala ya cheti cha uthibitisho wa ulipaji kodi (Tax Clearance Certificate)
5. Mwombaji asiwe amewahi kukutwa na hatia yoyote Mahakamani inayohusiana na utunzaji na uendeshaji wa ghala kwa mfumo wa stakabadhi ghalani.
6. Mwombaji asiwe amesababisha hasara yoyote ya uendeshaji wa ghala iliyopelekea migogoro kwa wadau wa mfumo wa stakabadhi ghalani.
7. Mwombaji awe na wadhamini watatu, akiambatanisha barua zao za utambulisho kutoka kwa mtendaji kata anakoishi kwa sasa.
8. Mwombaji aambatanishe nakala ya cheti cha uthibitisho wa mmiliki mwenye nguvu ya kisheria ( POWER OF ATTORNEY)
9. Mwombaji aambatanishe taarifa za kibenki za miaka miwili kuanzia Jan 2024 – Feb 2026.
10. Mwombaji awasilishe taarifa za fedha za miaka mitatu (3) Financial statements.
11. Mwombaji awe Kampuni/ Jina la biashara( Iliyosajiliwa na BRELA)
12. Mwombaji awe na uzoefu usiopungua miaka miwili wa kuendesha maghala makuu ya minada kwa mfumo wa stakabadhi ghalani.(Kiambatisho ni mikataba isiyopungua miwili ya kazi za uendeshaji ghala ya hivi karibuni, pamoja na nakala ya leseni kutoka bodi ya leseni za ghala (WRRB) zisizopungua miaka miwili iliyopita.
13. Waombaji wawasilishe zabuni zao ziliyosainiwa na mwanasheria "Nakala mbili ) nakala halisi moja na kopi moja zikiwa zimefungwa kwenye bahasha kwa umakini na kutiwa lakiri.
14. Mwombaji anatakiwa kulipa ada ya zabuni Tshs. **500,000/=** (Laki Tano tu) kwa kila zabuni atakayoomba "Hairudishwi" katika akaunti namba **0150267283200 (LINDI MWAMBAO COOPERATIVE UNION LTD) CRDB BANK,** na aambatanishe risiti pamoja na maombi yaliyofungwa katika bahasha.
15. Mwombaji aambatanishe cheti chake cha usajili wa mtoa huduma wa vyama vya ushirika Tanzania kinachotolewa na Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) .

16. Tangazo hili litadumu kwa muda wa siku 14 kuanzia 19 March 2026 – 01 April 2026.

17. Kablasha la zabuni linapatikana ofisi ya chama kikuu cha ushirika Lindi Mwambao baada ya kulipia ada ya zabuni kwa katibu bodi ya zabuni. Muda wa kupokea zanuni ni kuanzia saa 02:00 Asubuhi hadi 11:00 jioni kwa siku za kazi na Siku ya jumamosi ni saa 02:00 Asubuhi hadi 07:30 Mchana.

18. Maombi yote yafungwe kwa lakiri na yatumwe kwa katibu bodi ya zabuni Chama kikuu cha Ushirikia Lindi Mwambao na kuwasilishwa katika ofisi ya Chama Kikuu Lindi Mwambao. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 01/04/2026 saa 10:00 jioni na ufunguzi utafanyika mara tu baada ya muda wa kupokea zabuni kukamilika katika ukumbi wa ofisi ya chama kikuu cha Ushirika Lindi Mwambao-Mitwero.

**MAELEZO MENGINEYO:**

**Mwombaji aonyeshe mambo yafuatayo**

- **Anuani kamili ya kampuni &namba ya simu**
- **Mahali kampuni ilipo(Office location)**

LINDI MWAMBAO CO-OPERATIVE UNION LTD
AFF·LND·NO·2023·24
19 MAR 2026
P. O. BOX 140
LINDI

MENEJA MKUU,
CHAMA KIKUU CHA USHIRIKA
LINDI MWAMBAO - LTD,
S.L.P. 140,
LINDI.